**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI**

## SHULE YA SEKONDARI BUKAMA

S.L.P 01,
SHIRATI-RORYA
01/12/2023

Mkuu wa shule 0784784518
Makamu mkuu wa shule 0786180854

KUMB. NA. BSS/HWR/K1/2024

NDUGU MZAZI/MLEZI WA…………………………………………………………………...

SHIRATI-RORYA

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA JANUARI 2024

1. **UTANGULIZI**

Uongozi wa shule unayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Bukama mwaka **2024**.Hongera sana.

Fursa hii ni ya kipekee hivyo wewe kama mzazi/mlezi jitahidi kufanya maandalizi mapema ili mwanao aripoti siku ya kufungua na kuanza masomo.Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku ya **jumatatu** tarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni wiki mbili baada ya shule kufunguliwa..

2. **MAAGIZO MUHIMU**

**2.1 SARE ZA SHULE**

(i) Shati nyeupe **mbili (2)** zenye mikono mifupi **(TOMATO SHIRT)** kwa wote.(Wavulana na Wasichana)

(ii) Sketi **mbili (2)** moja rangi **nyeusi** na nyingine rangi ya **damu ya mzee** zote ziwe ndefu hadi chini kitambaa cha suti zenye kufunika vifundo vya miguu,marinda yasipungue 10 na yasizidi 20 na pindo liwe inchi 1.(Wasichana)

(iii) Suruali **mbili (2)** moja rangi **nyeusi** na nyingine rangi ya **damu ya mzee** zote zishonwe kwa kutumia kitambaa cha suti na ziwe na turn up ya sm16.Kamwe suruali aina ya modo hazitakiwi kabisa shuleni wakati wote. ( Wavulana )

(iv) Viatu vyeusi pea mbili (2) vya ngozi vyenye kufungwa na gidamu (kamba) na vyenye visigino vifupi kwa wote.( Wavulana na Wasichana )

(v) **Neck tie (**sio ndefu**)** moja rangi **nyeusi** na nyingine rangi ya **damu ya mzee**.

(vi) Soksi **nyeupe** ndefu **jozi tatu(3)** au zaidi kwa Wasichana.

(vii) Soksi **nyeusi** jozi tatu (3) au zaidi kwa Wavulana

(viii) Viatu vya michezo pea moja **(raba nyeusi)** kwa wanafunzi wote ( wavulana na wasichana )

(ix) Mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana tu.( Wavulana lazima wavae suruali kwa mikanda )

(x) Sweta moja rangi ya **dark-blue** kwa wanafunzi wote.

(xi) Hijab nyeupe kwa wanafunzi Waislam (Wasichana ) na zisizokuwa na urembo ivaliwe na suruali pana na nusu kanzu rangi nyeusi na damu ya mzee kulingana na ratiba ya sare ya shule siku husika.

**2.2 MAHITAJI YA KITAALUMA/DARASANI**

(i) Madaftari makubwa **tisa (9)-** counter books quire 3 au 4. Aje nayo yatakaguliwa siku ya kuripoti.

(ii) Madaftari madogo **tisa (9) -** msomi au aina nyingine kwa ajili ya mazoezi ya kila siku.Yatakaguliwa

(iii) Mkebe ( mathematical set)

(iv) Kalamu za wino mweusi au bluu za kutosha, penseli, ufuto,kichongeo na rula ya sm30.

(v) Aje na dictionary English – English ( Kamusi ya kiingereza) moja kwa matumizi yake.

(vi) Kila mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

(vii) Kwa ajili ya utunzaji wa mazingira kila mwanafunzi siku ya kuripoti aje na miche **miwili (2)** ataipanda na kuitunza muda wote atakaokuwa shuleni

**ZINGATIA**

(i) Siku ya kuripoti ni lazima mzazi au mlezi amlete mwanae shuleni na muda wa kuripoti ni **saa moja asubuhi** hadi **saa mbili asubuhi**, ikifika saa mbili asubuhi vipindi vinaanza hivyo wanafunzi wote wanatakiwa kuwa darasani.

(ii) Suruali nyeusi na sketi nyeusi zinavaliwa siku ya Jumatatu hadi Jumatano

(iii) Suruali damu ya mzee na sketi damu ya mzee zinavaliwa siku ya Alhamisi na Ijumaa.

(iv) T – shirt zinavaliwa siku ya jumatano na Ijumaa tu kwa wanafunzi wote.

(v) Raba nyeusi zinavaliwa siku ya ijumaa ambayo ndo siku ya michezo.

(vi) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuvaa au kuja na nguo ya aina yoyote ile hapa shuleni ambayo haikuagizwa katika fomu hii.

## 2.3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. **10** ya mwaka 1995 Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais -TAMISEMI YENYE JUKUMU LA Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

A) Heshima kwa viongozi,Walimu, Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima:
B) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima:
C) Kuhudhuria vipindi vyote darasani na kufanya mazoezi,majaribio na mitihani yote ni lazima.
D) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
E) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
F) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
G) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na kwa kufuata ratiba ni jambo la lazima.
H) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na Kutunza mali za umma.
I) Huruhusiwi kuwa na **simu, redio** wala **kamera** shuleni.

### 2.3.1 MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA SHULENI

(i) Kuvuta sigara.
(ii) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu pamoja na kufuga ndevu.
(iii) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule.
(iv) Kugombana.
(v) Kuiga mitindo ya kihuni mfano kunyoa kipara,kiduku, kupaka kucha rangi n.k.
(vi) Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
(vii) Kuzurura au kwenda nje ya shule bila kibali maalum au kutofika shuleni bila taarifa.
(viii) Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yoyote.
(ix) Kuwa na simu ,Kamera na redio shuleni.
(x) Kukiuka RATIBA au UTARATIBU wa shule.
(xi) Kutotii maagizo/maelekezo ya viongozi/walezi.
(xii) Kutembelea nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa.

### 2.3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:

A) Wizi.
B) Uasherati , ubakaji na Ushoga.
C) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi,kubeli na kadhalika.
D) Kupigana au Kupiga
E) Makosa ya jinai
F) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
G) Kudharau Bendera ya Taifa.
H) Kuwa mjamzito/Kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule.
I) Kuoa au Kuolewa.
J) Kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba.
K) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu.
L) Kukataa adhabu kwa makusudi.

M) Kutoroka Shule.
N) Kutokuwepo shuleni bila ruhusa kwa muda wa siku **30** mfululizo.
O) Kumiliki simu ya mkononi,redio au kamera.

**2.3.3 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi siku ya kuripoti.**

A) Medical Examination Form ambayo itahitaji mwanafunzi apimwe kikamilifu na kujazwa na Mganga wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Makamu mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.(Apimwe kikamilifu). Mzazi/Mlezi utoe taarifa sahihi za afya ya mtoto wako. Ikiwezekana vyeti vya matatizo ya kiafya kutoka kwa daktari vikabidhiwe Shuleni kwa ajili ya uthibitisho.
B) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai ikabidhiwe siku ya kuripoti.
C) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ikabidhiwe siku ya kuripoti.

**2.3.4 AFYA YA MWANAFUNZI.**

Mwanafunzi anapougua akiwa shuleni atapewa huduma ya kwanza tu na Shule , matibabu zaidi ni jukumu la mzazi. Hivyo basi unashauriwa kumwandalia mwanao kadi ya **Bima ya afya** inayofanya kazi kwa ajili ya matibabu zaidi hospitali ili kupunguza gharama zisizo za lazima.

..........................................

**RICHARD B OKORE**

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI BUKAMA**

THE HEADMASTER
BUKAMA SECONDARY SCHOOL
01 DEC 2023
P. O. Box 01 SHIRATI
RORYA - MARA




**KARIBU BUKAMA SEKONDARI**



**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI**

# SHULE YA SEKONDARI BUKAMA

S.L.P 01,
SHIRATI-RORYA
01/12/2023

Mkuu wa shule 0784784518
Makamu mkuu wa shule 0786180854

KUMB. NA. BSS/HWR/K1/VOL 1/2024

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili………………………………………………………………………
2. Jina la shule ya msingi uliyosoma …………………………………………………..
3. Namba yako ya mtihani ya darasa la saba ………………………………………….
4. Tarehe ya kuzaliwa: tarehe ………… mwezi …………… mwaka …………………………..
5. Mahali ulipozaliwa: Wilaya …………………………… Mkoa …………………………………
6. Kabila …………………………………Taifa …………………………………………………….
7. Dini /dhehebu ……………………………………………….
8. Jina la baba ……………………………………………Taifa …………………………………….
9. Anuani ya baba (Anapoishi) ………………………………………………………………
10. Namba za simu za baba ………………………………., ………………………………………….
7. Kazi ya baba ………………………………………………………………………………..
8. Jina la mama ………………………….. Kazi yake …………………………………………………
9. Namba za simu za mama …………………………….., ………………………………….
10. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana …………………………………………
11. a) Jina na anuani ya mlezi wako kama si mzazi

    ………………………………………………………………………………………

    ………………………………………………………………………………………

    b) Kama ni mlezi uhusiano wako naye ……………………………..

    c] Namba za simu za mlezi wako ……………………………………, ……………………
12. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (taja sehemu moja tu utakayokwenda kila wakati. …………………………………………………………
13. Nathibitisha kwamba taarifa zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

    Saini ya Mwanafunzi.........................................Tarehe …………………………….

    Saini ya Mzazi ………………………………………….Tarehe …………………..…………

***Fomu hii ni lazima ijazwe na kukabidhiwa ofisini siku ya kuripoti***

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI**

## SHULE YA SEKONDARI BUKAMA


S.L.P 01,
SHIRATI-RORYA
01/12/2023

Mkuu wa shule 0784784518
Makamu mkuu wa shule 0786180854


KUMB. NA. BSS/HWR/K1/VOL1/2024

### FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

1. **Sehemu ya Mwanafunzi**

Mimi…………………………………………………………………………………………………

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka ……………

Katika shule ya sekondari ya Bukama na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za Nchi.Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya Elimu ya kujitegemea na sitamiliki simu ya mkononi,redio na kamera wala kushiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni

Sahihi ya Mwanafunzi…………………………………Tarehe …………………

2. **Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi…………………………………………………………………Ninakubali mtoto wangu …………………………………………… Kujiunga kidato cha kwanza shule ya sekondari Bukama mwaka ………………………Nina ahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa na hatamiliki simu ya mkononi awapo shuleni wala kushiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa muda wote atakapokuwa mwanafunzi. Nitashiriki kufuatilia maendeleo yake mara kwa mara,kumhimiza kusoma kwa bidii na kusimamia nidhamu yake kikamilifu.

Anuani yangu ni …………………………Simu Na …………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Yafuatayo ni Majina ya watu watatu ambao Mawasiliano ya kiofisi yanaweza kufanyika kuhusu mwanafunzi huyu;

| JINA (*Majina Matatu*) | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

**Ninaahidi kuwa Mwanangu/Mwanafunzi akishindwa kupata daraja la 1 au la 2 au la 3 kwenye mitihani ya kumaliza mwaka (annual examination) nitakuwa tayari kumuhamishia shule nyingine.**

***Sahihi…………………………………***  ***Tarehe ……………………………***

***Fomu hii ni lazima ijazwe na kukabidhiwa ofisini siku ya kuripoti.***

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

**BUKAMA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS**

Student's full name……………………………………………………………………………………...

Age………………………Height (in cm)……………………………Weight………………………………..

1. Blood count………………………………………(Red and White)…………………………………….
2. Stool examination…………………………………………………………………………………..
3. Urine analysis……………………………………………………………………………………….
4. Syphilis and other V.D……………………………………………………………………………...
5. T.B and Leprosy Test……………………………………………………………………………….
6. Eye test……………………………………………………………………………………………...
7. Ear test……………………………………………………………………………………………
8. Chest test…………………………………………………………………………………………
9. Abdominal test……………………………………………………………………………………...
10. Plano test (Girls)…………………………………………………………………………………….
11. Spleen……………………………………………………………………………………………….

Additional information e.g Physical defects of impairments infection, chronic or family diseases (e.g sickle cell) inability to eat certain foods etc.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above student is fit/is not fit to pursue Secondary education.

Signature…………………………………………………………………………………….

Designation………………………………………………………………………………….

Station……………………………………………………………………………………….

Date………………………………………………………………………………………….